


# Matibabu ya COVID-19

Swahili 12/2022

## Ni nini?

Dawa zinapatikana ili kukusaidia kupambana na maambukizi ya COVID-19 ikiwa ni pamoja na tembe za kutibu magonjwa yanayosababishwa na virusi. Matibabu haya yanaweza kukusaidia usipate maradhi makali na kuhitaji kulazwa hospitalini, lakini sharti uyapokee haraka iwezekanavyo baada ya dalili zako kuanza. Kupata chanjo bado ndio njia bora zaidi ya kuzuia COVID-19.



## Je, yanaweza kunisaidia?

Unaweza kustahiki kupata matibabu haya ikiwa umepatikana kwamba una COVID-19, uko katika hatari kubwa ya kupata maradhi makali, na dalili zako zilianza hivi karibuni. Hata watoto wenyewe umri mdogo wa siku 28 walio katika hatari kubwa ya kupata maradhi makali wanawenza kustahiki kupata matibabu. Zungumza na daktari ili ujue ikiwa matibabu haya yatakuwa salama na yanafaa kwako na mtoto wako.

## Je, ninapaswa kupata matibabu lini?

Dawa hizi hufanya kazi vyema zaidi ikiwa utazitumia punde tu baada ya kuanza kujihisi mgonjwa. Unahitaji kuanza kutumia tembe za kupambana na virusi ndani ya siku 5 za kwanza baada ya kuibuka kwa dalili. Ni muhimu kupata kipimo cha virusi vya COVID-19 mara moja ikiwa una dalili ili uweze kutumia dawa hii. Pata kituo cha kufanyiwa kipimo kilicho karibu nawe kwa kutembelea <https://coronavirus.utah.gov/testing-and-treatment>.



## Je, yanatilewa vipi?

Matumizi ya tembe za kupambana na virusi huagizwa na daktari na tembe hizo humezewa nyumbani mara 2 kwa siku kwa siku 5. Ni watoa huduma za afya waliodhinishwa na waliopokea mafundisho tu wanaoweza kukuandikia agizo la kutumia tembe za kupambana na virusi.

## Je, ni salama?

Dawa hizi zimeidhinishwa na Mamlaka ya Taifa ya Dawa (FDA), na zimedhihirishwa kuwa ni salama na zinafanya kazi kuitia majoribio ya kimatibabu. Dawa na matibabu yote yana athari zinazoweza kutokea. Zungumza na daktari au mtoa huduma za afya anayekupa dawa hizi ikiwa una wasiwasi kuhusu athari zinazotokana na matibabu, pamoja na mambo unayofaa kuangalia.



**Je, nitayapata wapi?** Mtoa huduma wako wa matibabu ya msingi, ofisi za madaktari, kliniki za matibabu ya dharura, hospitali, na maduka ya dawa kote katika jimbo yanaweza kukupa dawa hizi. Zungumza na daktari ili ujue kama dawa hizi zinakufaa. Unaweza kutozwa ada au bima yako ikatumiwa bili ya gharama ili uweze kupata matibabu haya.

Tembelea [coronavirus.utah.gov/treatments](https://coronavirus.utah.gov/treatments) au upige simu kwa Idara ya Utah ya Afya na Huduma za Binadamu kuitia 385-273-7878 ili kupata orodha ya maeneo ambayo unaweza kupata matibabu haya.